

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA AROBAINI NA SITA**

**09 JUNI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA SITA – TAREHE 09 JUNI, 2026

I. DUA:

II. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**541. MHESHIMIWA ENG. CHACHA MWITA WAMBURA  
(GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itabuni na kutekeleza miradi mikubwa ya uzalishaji mali Geita Mjini ili kuongeza vyanzo mbadala vya mapato.

**542. MHESHIMIWA JUMA KAWAMBA MUSTAFA  
(IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja kati ya Kijiji cha Vumilia na Itulu kutokana na changamoto ya kujaa kwa Mto Wara wakati wa masika.

**543. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Tumbi - Kipera - Itema ili kuondoa changamoto ya usafiri kwa Wananchi wa Kata ya Tumbi.

**544. MHESHIMIWA ENG. FADHILI SANDALI CHILOMBE (TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti Makorongo yaliyotokana na Maji ya Mvua katika Vijiji vya Nalasi na Mchoteka.

**OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):**

**545. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUWAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Vijana wenye Vikundi vilivyosajiliwa na wenye Mahitaji Maalum.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**546. MHESHIMIWA LUCY EDWARD MWAKYEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali kwa kushirikiana na Majukwaa ya Kimataifa na Kamati za Kitaifa itasimamiaje uchakataji wa taka na matumizi ya Nishati kwenye hoteli.

**WIZARA YA UJENZI:**

**547. MHESHIMIWA KASSIMU AMARI MBARAKA (TANGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza Ujenzi wa Barabara ya Soni, Mbelei, Kwalei, Kwehangala, Bumbuli hadi Dindira Km 74 kwa kiwango cha lami.

**548. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE  
(LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kutoka Kibena hadi Madeke Kilomita 126 kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA KILIMO:**

**549. MHESHIMIWA DEVOTHA DANIEL  
MBURARUGABA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha kilimo Mkoani Kagera kutoka kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha viwanda na kuongeza thamani ya mazao.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**550. MHESHIMIWA DICKSON NATHAN LUTEVELE  
(MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Sheria itamtambua Mwanamke kuwa mrithi halali wa mali za Familia sawa na Mwanaume.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**551. MHESHIMIWA DKT. YAHAYA ESMAIL NAWANDA (NEWALA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Chuo cha VETA katika Mji wa Kitangari.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**552. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itawekeza Fedha kwenye Jeshi la Zima Moto Wilayani Urambo.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**553. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali haioni haja ya kuzipa Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam mamlaka ya kushughulikia masuala ya ardhi ikiwemo utoaji wa Hati za umiliki.

**DODOMA**  
**09 JUNI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD**  
**KATIBU WA BUNGE**

